

# Mambo Unayopaswa Kujua Kuhusu Haki Zako Kazini nchini Marekani



**Una haki kazini. Jifunze sheria zinazokulinda na jinsi ya kutambua unyanyasaji au kutumiwa vibaya mahali pa kazi.**

## HAKI ZANGU NI ZIPI?



- Lazima ulipwe **angalau mshahara wa chini uliowekwa** katika jimbo unakofanya kazi. Katika majimbo mengi, mshahara wa chini ni wa juu kuliko mshahara wa chini wa kitaifa (\$7.25 kwa saa).
- Ikiwa unafanya kazi zaidi ya saa 40 kwa wiki, anayekupa kazi lazima akulipe malipo **ya saa za ziada**. Hii ina maana kwamba lazima wakulipe mara moja na nusu ya kiwango chako cha kawaida cha malipo kwa kila saa unayofanya kazi zaidi ya saa 40 kwa wiki.

- Sheria za kitaifa pia zinamtaka mwajiri wako kuhakikisha unafanya kazi katika mazingira **salama na yenye afya**.
- **Ulinzi kwa vijana:** Vijana walio chini ya umri wa miaka 18 hawaruhusiwi kufanya kazi zinazochukuliwa kuwa hatari, kama vile uchimbaji wa madini, kutumia mashine nzito, kufanya kazi juu ya paa, au kuendesha magari. Pia kuna sheria zinazoweka mipaka ya idadi ya saa ambazo vijana wanaruhusiwa kufanya kazi.

## KUPATA KIBALI CHA KAZI

- Kwa vijana wakimbizi na vijana wengine wanaostahiki huduma za ORR nchini Marekani, ni muhimu kuelewa kwamba **unaweza kufanya kazi tu ikiwa una kibali cha kisheria cha kufanya kazi**. Ikiwa bado hujapokea kibali chako cha kufanya kazi, huruhusiwi kisheria kufanya kazi mpaka utakapokipokea.
- Ni bora **kuzungumza na wakili mwenye ujuzi wa masuala ya uhamiaji** ili ujifunze zaidi kuhusu chaguo zako za kupata kibali cha kufanya kazi nchini Marekani.
- Kufanya kazi bila kibali cha kisheria inaweza kuwa na **hatari kubwa**:
  - Inaweza kusababisha matatizo ya baadaye na mamlaka za uhamiaji au katika kesi yako ya kisheria.
  - Kufanya kazi bila kibali cha kisheria inaweza kukuweka katika hatari kubwa ya kutumiwa vibaya, kunyanyaswa, au kudhulumwa na wanaokupa kazi.



## DALILI KUMI ZA ONYO ZA KUTUMIWA VIBAYA NA KUNYANYASWA KAZINI



- 1 Ikiwa anayekupa kazi hakulipi mshahara wa chini uliowekwa katika jimbo lako;
- 2 Ikiwa unafanya kazi zaidi ya saa 40 kwa wiki, na anayekupa kazi hakulipe malipo ya saa za ziada;
- 3 Ikiwa anayekupa kazi hakuruhusu mapumziko ya kula au kwenda chooni wakati wa siku ya kazi;
- 4 Ikiwa anayekupa kazi hakuruhusu kuchukua siku ya mapumziko wakati;
- 5 Ikiwa anayekupa kazi anakutishia kwamba utapoteza kazi yako ikiwa utachukua siku ya mapumziko;
- 6 Ikiwa anayekupa kazi anashikilia nyaraka zako za utambulisho (kama pasipoti yako, kibali cha kazi, au kadi ya usalama wa jamii) na hakuruhusu uzipate;
- 7 Ikiwa anayekupa kazi anakata pesa kutoka kwenye mshahara wako ili kulipia kodi ya nyumba au gharama nyingine, au kulipa deni;
- 8 Ikiwa anayekupa kazi anakutishia kupiga simu polisi au mamlaka ya uhamiaji kwa sababu ya kufanya kazi bila kibali cha kisheria;
- 9 Ikiwa anayekupa kazi anakudhuru au anakutishia kukudhuru wewe au familia yako usipo fanya kazi;
- 10 Ikiwa unajisikia kulazimishwa kufanya kazi kwa sababu ya hofu ya kuumizwa.



Ikiwa unajikuta katika hali kama hiyo, zungumza na mtu mzima wa kuaminika, msimamizi wako wa kesi, au wakili mwenye sifa stahiki. Unaweza kupiga simu kwenye nambari ifuatayo kwa msaada na taarifa kuhusu rasilimali, haki na manufaa yako, na kuomba ufikivu wa rasilimali zinazopatikana:



**Nambari ya Simu ya  
Kibinadamu ya Kitaifa**

**1-888-373-7888**